# Kanisa la Mungu Katika Utaabiri

**Yesu Kristo alisema kuwa Kanisa la Mungu litasimama imara hadi mwisho wa nyakati hizi. “Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote,” Kristo anawaambia wanafunzi wake wa kweli, “hata ukamilifu wa dahari” (Mathayo 28:20). Nyakati zijazo zina msimamo gani kwa Kanisa la Kristo?**

Yesu Kristo aliahidi kulijenga kanisa lake, na wala “milango ya kuzimu haitalishinda” (Mathayo 16:18). Na kwa kweli, Yesu alililijenga Kanisa lake. Alianza kulijenga katika karne ya kwanza baada ya kifo chake, alipowaita na kuwafunza wanafunzi wake wa kwanza, na kuwatuma kuihubiri injili ya ufalme wa Mungu kwa mataifa yote.

Lakini ni “kanisa” gani Yesu alisema atalijenga?  “Kanisa” lina maanisha nini? Watu wengi wanafikiria kuhusu mijengo mirefu yaliyo na dirisha za vioo vilivyo na rangi tofauti wanaposikia neno “kanisa.” Au, wanafikiria kuhusu mazoezi ya “kidini”, kama vile shule ya watoto siku ya Jumapili, ibada siku ya Jumapili inayohusisha maombi, mafunzo, na mahubiri.

Neno la Kiyunani linalo tafsiriwa “kanisa” katika Agano Jipya halikulazimika kuwa ushirika wa kidini, lakini uliweza kuwa aina yeyote ya mikutano. Ungeweza kuwa “mkutano mjini”, umati wenye hasira, ushirika ya wanaoabudu katika sinagogi, au mikutano ya aina yeyote. Neno eklesia (inayosimamia mambo ya kikanisa),  kwa kinaga ubaga humaanisha “mkutano.”

Kwa hivyo Yesu alisema ataliita ushirika la waaminio watakao eneza injili yake ya kweli kwa ulimwengu na kuwa kama washahidi kwa mataifa yote. Hata hivyo, Agano Jipya inaonyesha kuwa ushirika wa kweli wa Kristo – Kanisa la kweli la Mungu – haikatataliwi kuwa katika eneo au mipaka zozote, lakina linahusisha wote ambao Roho wa Mungu anakaa ndani yao.

Kwa washirika wa kanisa la Roma, Mtumishi Paulo anaandika, “Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamfuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake” (Warumi 8:9). Mtu yeyote asiye na Roho wa Kristo ndani yake siyo wa Kristo. Na kama si wa Kristo, yeye sio mshirika katika ushirika wa Kristo, ambayo ni “Kanisa la Mungu aliye hai” (1 Timotheo 3:15).

**Msingi wa Kanisa la Kristo**

Kristo alianza kuweka msingi wa kanisa lake alipowaita wanafunzi wake wa kwanza. “Nifuateni,” Aliwaambia wavuvi (Petro na Andrea), “nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu” (Mathayo 4:19). Kwa maneno mengine, Petro na Andrea, pamoja na mitume wengine Yesu atakaowaita, watakuwa kama vyombo vitakavyotumiwa na Kristo kulijenga Kanisa lake. Kama vile wavuvi walivyotupa jarife baharini na kuvua samaki wengi, watumishi wa Yesu vile vile wataieneza injili ya ufalme wa Mungu kote ulimwenguni, na ujumbe wa ufalme itawaleta wengi wa wanadamu katika ushirika ya waaminio kwa Kristo.

Yesu Kwanza aliwaita wanafunzi kumi na wawili, na kuwaongeza wanafunzi wengine wengi ili kuliunda kundi kubwa litakalokuwa msingi wa waaminio kwa nyakati ujao. Baada ya ufufuo wake, na kabla ya kuwaleta wengi katika ushirika wa waaminio, Kristo aliwatokea wengi ambao aliwachagua kama msingi wa viongozi na akawavuvia na kuwaambia “pokeeni Roho Mtakatifu”, (Yohana 19:22).

Mitume waliipokea Roho Mtakatifu papo hapo. Punde tu siku chache awali Kristo alikuwa amewaambia kuwa Roho Mtakatifu “anakaa kwenu naye atakuwa ndani yenu [katika siku zijazo] ” (Yohana 14:17). Wakati huo, Roho alikuwa na wanafunzi bora Yesu (aliyekuwa na Roho bila ya kipimo – Yohana 3:34) alikuwa nao, lakini atakaa nao hivi karibuni na itawapa uwezo wa kipekee, itakayowawezesha kuitimiza kazi ya Kristo, “Enenedeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi” Mathayo (28:19,20).

Hivyo, msingi wa kanisa la Agano jipya likakamilika. Wanafunzi wa kwanza walichaguliwa na kutayarishwa kwa maisha ya kazi ya kikristo. Hivi karibuni Mungu atawaongeza maelfu katika ushirika upya ulioanzishwa na Kristo.

**Sehemu ya Pili: Kumwagwa kwa Roho**

Wimbi la kwanza wa ajabu ulikuwa siku ya Pentekoste, wiki saba baada ya kifo na ufufuo wa Kristo.

“Siku ya Pentekoste ilipowadia, Wao [wanafunzi – jumla ya majina ilipata mia na ishirini – Matendo ya Mitume 1:15] walikusanyika pamoja. Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingi, kama Roho alivyowajalia kutamka” (Matendo ya Mitume 2:1-4).

Hatimaye, kazi ya miujiza wa Roho uliwavuta wengine waliokuwa Yerusalemu kwa sherehe.

“Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika , wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?’….Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, Maana yake ni nini mambo haya? (Matendo ya Mitume 2:5-12).

Wakati mtu alipofikiria kuwa labda wanafunzi walikuwa wamekunywa divai mingi, Petro akasema:

*Sivyo manvyodhani, watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana;Lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli: Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu; na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri….Na itakuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa’ ”(aya ya 15 - 21).*

Maneno za Petro hakuyasema bila ya sababu. Roho ilitumia maneno ya mitume kwa kuwaongoza wengi kuona makosa za njia yao na kurudi kwa Mungu kwa kutubu na mioyo yao yote na kumkumbatia Yesu kama Mwalimu tena Masihi. Nao

waliopokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu (aya ya 41).

Katika siku zilizofuata, maelfu waliongezeka katika ushirika ya waaminio (Matendo ya Mitume 2:47, 4:4). Yesu alikuwa akilitimiza ahadi yake. Alikuwa akilijenga kanisa lake!

**Je, Utaabiri wa Yoeli Ulitimizwa 'mara moja na kwa wakati wote'?**

Utaabiri mingi kwenye maandiko zinaweza kutimizwa mara moja tu. Zikitimizwa, hayawezi kutimizwa mara ya pili. Mifano yanaweza kupatikana katika Agano la Kale na vile vile katika Agano Jipya: Utaabiri wa Isaya kuhusu kuteseka na kifo cha Masihi (Isaya 53) ilitimizwa mara moja wakati wa kuteseka na kufa kwa Yesu, na haitaweza kutimizwa tena katika matukio mengine ya kuteseka na kufa. Utaabiri wa Yesu kuhusu wakati wa Dhiki kubwa "ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu  hata sasa, wala haitakuwepo kamwe" (Mathayo 24:21) haiwezi kuwa na kutimizwa kimoja.

Lakini sio taabiri zote kwenye maandiko zinalazimika kuwa na kutimizwa kimoja kikamilifu kwa wakati mmoja na eneo. Utaabiri wa Yoeli wa kumwagwa kwa Roho wa mungu ni utaabiri kama huo. Ilitimizwa kwa kiwango fulani katika karne ya kwanza Kanisa la Agano Jipya lilipoundwa, lakini ahadi ya Mungu wa kumwagwa kwa Roho kwa "miili yote" haijakamilika!

Wakati unakuja ambapo Mungu ataumwaga Roho wake tena; ambapo tukio za miujiza za ajabu zitatokea; vilema watatembea, vipofu wataona, na viziwi watasikia; ambapo maelfu watarudi kwa Mungu kwa kutubu mioyoni mwao, vile walivyofanya siku ya Pentekoste katika karne ya kwanza.

**Kile ambacho kanisa la wakati wa mwisho kinaweza kutarajia**

Kama ilivyosemwa hapo awali, aliwaahidi wanafunzi wake wa kweli kuwa atakuwa nao "hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20). Kwa sababu wanafunzi wake wa kwanza walikufa karne mingi zilizopita, Yesu (kupitia Roho Mtakatifu), kwa kuweka ahadi yake, huenda alikuwa na kila kizazi kilichofuata wa wanafunzi wa kweli kupitia miaka 2000. Bado ako na wanafunzi hadi leo, na jinsi alivyoahidi, atakuwa nao hadi ukamilifu wa dahari.

Yesu, akiongea kuhusu wakati ambapo hatakuwa kamwe katika mwili, anawaahidi wanafunzi kuwa atakuwa nao katika Roho. “Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu” (Yohana 14:18). Aliendelea kuahidi, “Mtu akinipenda atalishika neno langu; na Baba yangu atanipenda, nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake” (aya ya 23)

Naam, Mungu Baba na Yesu Kristo watakuwa na watu wa Mungu katika hii ulimwengu (Ufunuo 21-22). Lakini katika somo lilioko hapo juu Yesu anaongea kuhusu Baba na mwana wakikaa kiroho ndani ya kanisa. Hii ni njia nyingine ya kusema “sitawaacha watu wangu yatima; nitakuja kwao na kuwa nao, nikiwaendeleza na kuwainua, hadi mwisho wa dahari, wakati nitarudi tena na kuwasanya katika Ufalme wangu wa milele”.

Paulo alisema kwa kanisa la Wakorintho, “kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu alivyosema: ‘Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu’ ” (2 Wakorintho 6:16).

Kanisa ni “hekalu la Mungu aliye hai” kwa sababu palipo na kanisa, Mungu yupo. Kristo ako na wanafunzi wake kila mara – kama alivyoahidi.

Hii yote ina maana gani?

Kama Yesu alivyowaahidi wanafunzi wake wa karne ya kwanza kuwa hatawaacha wala kuwapuuza, kuwa atawaongoza kupitia Roho Mtakatifu, na kuwa atakuwa nao hadi mwisho wa dahari, basi tunaweza kutarajia kuwa atakuwa na, kuisaidi na kuhamashisha kanisa la nyakati wa mwisho jinsi alivyowafanyia wanafunzi wake wa kwanza.

Mungu mara kwa mara hutoa washahidi tosha kabla ya kumwaga hamaki yake juu ya mwenye dhambi. Aliwatuma nabii kwa Israeli wa jadi, na kuwaonya watu kutoka kwenye dhambi ili kurudi kwa Mungu kwa kutubu, au kupewa adhabu zinazoogopesha na Mungu mwenye hasira.

Yesu aliwaambia wayahudi wa nyakati wake ambao hawakuamini, “Kwa sababu ya hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawauwa na kuwasulubisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; hivyo iwe juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki,

hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. Amin, nawaambieni, mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki. (Mathayo 23:34-36)

Kati ya miaka 40 ya ilani ya Kristo, Yerusalemu ilishindwa na majeshi ya Tito na hekalu likaharibiwa – lakini sio bila ya mshahidi mwenye nguvu. Kutokea siku Roho ilimwagwa kutoka mbinguni, tukio la miujiza kimoja cha ajabu baada ya nyingine ilitendeka mikononi mwa mitume. Vilema walitembea, vipofu walipata kuona, wagonjwa waliponywa, na shetani alishindwa. "Na kwa mikono ya mitume zikafanyika ishara na maajabu mengi katika watu" (Matendo ya Mitume 5:12).

Ujumbe kuu la mitume (kuwa "huyo Yesu mliyemsulubisha" ni " Bwana na tena Kristo" Matendo ya Mitume 2:36) iliyofuatwa na ilani ("Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi" - aya ya 40) na kuthibitishwa kwa nguvu za ishara za ajabu pamoja na kumwagwa kwa Roho.

Nyakati zijazo – pengine hivi karibuni – Mungu atakuja kati ya shughuli za ulimwengu huu. Atasababisha vita dhidi ya waovu, na kumtuma Yesu Kristo katika hii ulimwengu ili kuihukumu mataifa, kushinda adui zake, na kuiweka Ufalme wake.

Je, tunatarajia kuwa nyakati kama huo utafika bila ya ushahidi halisi? Je, tunafikiria kuwa nyakati za kuthibitishwa kwa ujumbe zimepita?

La! Ahadi ya Mungu wa kumwaga Roho wake haikukamilika katika siku za mitume. Tuko na kila sababu kuamini kuwa ataimwaga Roho wake tena na kufanya kazi za miujiza kupitia watumishi wake. Mara nyingine, vipofu watapata kuona, viziwi watasikia, na viwete watatembea. Mara nyingine tena, ishara za ajabu na miujiza zitatendwa mikononi mwa watumishi wa kweli wa Mungu.

Kama vile utaabiri wa Yoeli unavyosema, "Na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Roho yangu, nao watatabiri" (Matendo ya Mitume 2:17,18). Ndoto za unabii na maono ni sehemu ya ishara na maajabu zinozofuatwa na kumwagwa kwa Roho.

Sehemu nyingine wa utaabiri unasema zaidi kuwa kumwagwa kwa Roho (pamoja na ishara na miujiza) haikutimizwa kikamilifu nyakati za mitume. Maandiko linaendelea:

Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini, damu na moto, na mvuke wa moshi. Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja ile siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri. Na itakuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokolewa (aya ya 19-21).

Tazama kwamba kumwagwa kwa Roho ina uhusiano wa ajabu katika mbingu na ishara katika nchi chini kabla ya kuja ile "siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri" Hii inaweza sema tu kuhusu mwisho wa dahari – wakati utakao ongoza hadi kurudi ya pili wa Yesu Kristo.

Ni wazi kwamba, ahadi ya Mungu wa kumwaga Roho wake "kwa miili yote" haikukamilika nyakati ya mitume. Kama kutimizwa wa karne wa kwanza ni maonyesho ya kutimizwa wa nyakati za mwisho wa utaabiri huu, basi hii ndio tunaweza kutarajia katika siku zijazo: Kanisa la Mungu litaendelea kwote. Maelfu watarudi kwa Mungu kwa kutubu, watabatizwa kwa maondoleo ya dhambi, na kupokea tuzo za Roho Mtakatifu. Miujiza za ajabu zitatendeka, pamoja na kuponywa kwa magonjwa mengi, kuondolewa kwa shetani, na pengine ufufuo wa wafu. Haya yote yalitendeka wakati wa Kristo na mitume; hakuna haja kufikiria kuwa hayata tendeka tena, na haja kufikiria kuwa yatatendeka.

**Kanisa Kulikamilisha Jukumu**

Kristo aliyefufliwa aliwaamuru wanafunzi wake kwenda kila mahali wakieneza ujumbe nzuri wa ufalme wa Mungu.

"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (Mathayo 28: 18-20).

Tazama kweli ambazo zimetajwa hapa: Kwanza, Yesu anawahakikishia wanafunzi wake kuwa anayo mamlaka yote mbinguni na duniani. Ya pili, anawaamuru wanafunzi wake kuenenda kila mahali kuieneza injili kisha kuwafanya wanafunzi.

Ya tatu, anatoa ahadi kwa wanafunzi wake kuwa atakuwa nao siku zote hadi mwisho wa dahari.

Hizi kweli tatu, yakiangaliwa kwa ukamilifu, yanamaanisha kuwa Yesu, aliye na mamlaka mbinguni na duniani atawasaidia na kuwaongoza wanafunzi wake wa kweli wakitii amri yake kuenenda na kufanya wanafunzi kwa mataifa yote. Hii inamaanisha Kuwa kazi ya kanisa la kweli la Mungu siyo kazi ya wanadamu, bali ni kazi ya Yesu Kristo aliye hai!

Yatafakari hayo. Kama watu wa Mungu leo wanakosa kuitii amri ya Kristo ya kuihubiri injili na kuenenda kufanya wanafunzi – kama wanaichukua amri (Mathayo 28:19,20) kutumika kwa wanafunzi wa karne ya kwanza au kujiwia radhi kwa kusema kuwa kuwa washahidi wawili wa Ufunuo 11 watalitimiza – basi Kristo atamtafuta mtu mwingine kuifanya kazi!

Ni aidha njia moja au lingine, kazi ya Mungu itatimizwa. Kristo mwenyewe alitaabiri kuwa kanisa lake litafaulu kikamilifu kulitimiza amri yake.

Hebu tutazame kile Yesu alisema wakati wanafunzi wake walimwuliza kuhusu “ishara” za Kurudi kwake na kuhusu mwisho wa dahari:

“ Yesu akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi. Nanyi mtasikia habari za vita na matesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu. Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawauwa; nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. Ndipo wengi watakapojikwaa, nao watasalitiana, na kuchukiana. Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi. Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa. Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. Tena habari njema ya ufalme utahubiriwa katika ulimwengu wote, kwa ushuhuda wa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja” (Mathayo 24:4-14).

Tazama kwamba Yesu anawajulisha wanafunzi wake kuhusu hali kadhaa kabla ya dhiki ya mwisho na kurudi ya pili. Kwanza, wanafunzi wa kweli watasalitiwa na

hata kuuliwa. Pili, manabii wa uongo watatokea – labda kutoka ndani ya kanisa – na kuwasaliti na kuwadanganya wengi. Lakini hata ingawa hali hizi zitatokelezea, Yesu anasema, kanisa la kweli litafaulu kutimiza kikamilifu amri ya kuihuburi injili kwa mataifa yote.

Mathayo 24 inasema kuhusu aina mbili ya dhiki: "dhiki kubwa" inayofuatwa na kutokelezea wa "chukizo la uharibifu" ndani ya Yerusalemu (aya ya 15-21); na dhiki ambayo watakatifu watapata (aya ya 9). Hili limejirudia karne baada ya karne, na itaendelea hadi mwisho wa dahari. Hata hivyo, Yesu anataabiri kufaulu kwa kanisa la mwisho. Injili itahubiriwa mbali na tena pana; Kanisa litatimiza amri yake.

Utakatifu wa mwisho utafunuliwa wakati "muhuri ya tano" litakapofunguliwa:

"Na alipoifungua [Mwana kondoo - Kristo] muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. (Ufunuo 6:9).

Hawa ndio waliokuwa wakristo watakatifu, au pengine watakatifu wote kuanzia siku za mitume hadi sasa. Kama damu ya Habili mwenye haki ikililia Mungu kutoka kwenye ardhi (Mwanzo 4:9), roho za watakatifu zikimlilia Bwana kwa sauti ili kuweza kupata haki: "Ee Mola, Mtakatifu, mwenye kweli, hata lini kutohukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi?" (Ufunuo 6:10).

"Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao" (aya ya 11).

Wale wanaokaribia kuuliwa wanaitwa "wajoli" na "ndugu" za watakatifu wa jadi, waliotoa maisha yao kwa ajili ya neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda [injili ya kweli] walio nao." Wao ndio kizazi cha mwisho wa wakristo watakatifu. Kama wenzao, watatoa maisha yao kwa ajili ya neno la Mungu na kwa ujumbe wa Kristo na Ufalme wake.

Kumbuka, wakati usaliti uliingia kwa kanisa la jadi, injili iliweza kuenea katika eneo zingine na idadi ya wanafunzi ikaongezeka. Tunaweza kutarajia chochote tofauti nyakati za mwisho?

**Hakuna "Unyakuzi"**

Leo, wazo la kuepuka dhiki ya mwisho kwa njia ya "unyakuzi" imeenea kwa wahubiri wengi, lakini Bibilia inafunza kuwa hakuna funzo kama hilo. (Kwa kisomi hiki, tuandikie ili uweze kupata kitabu, Je, tuitarajie Unyakuzi'?). Badala yake, Agano jipya linaonyesha kuwa wakristo waliobadilika kweli – wanaume na wanawake wenye imani kabisa, waliojawa na Roho wa Mungu, na wanaotarajia na kutamani kurudi kwa Bwana yao, bado watakuwa duniani wakati yule "mwenye dhambi" atakapojitokelezea (2 Wathesalonike 1:1-2:12).

Usifanye makosa, kanisa "litafikiwa" kumkaribisha Kristo atakaposushwa kutoka mbinguni (1 Wathesalonike 4:15-17), lakini tukio hili litatokea miaka michache baada ya yule mwenye dhambi kuja kwenye jukwaa.

Tazama tukio zinazozunguka Kurudi ya Pili kwa Yesu Kristo:

1. Watakatifu wenye imani wateswao watapata raha wakati wa kufunuliwa kwa Kristo (2 Wathesalonike 1:7).
2. Waovu – " wale wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo" – wataadhibiwa wakati wenye imani watapata raha (aya ya 7-9).
3. Yule mwenye dhambi atamalizwa kwa ufunuo wa kuwapo kwake – (2 Wathesalonike 2:8) – hiyo ni kabla ya tukio mbili za kwanza kutokea.

Kwa kweli, tuzo la watakatifu na adhabu kwa waovu zinahusika sawa na tukio hili – "wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni" (1:7), "atakapokuja siku hiyo" (1:10), "kwa ufunuo wa kuwapo kwake" (2:8). Tukio hizi hazina nafasi ya hisia za siri na zenye furaha.

Utafiti wa kweli unafunua kuwa maandiko hayaoni watakatifu waliobaki, au wanaume na wanawake waliobadilika baada ya Kristo kuja kwa siri kwa kanisa. Mukatadha huu unadukuliwa hapa. Paulo anawaongelesha watakatifu waaminifu wa kanisa la Wathesalonike (na kwa uhusiano, Kanisa la Mungu kwa ujumla), sio kwa wasiobadilika au waliobadilika kwa kiwango fulani. Sikiza maelezo yake, na uangaliee kama hii inakaa kama kutokuwa na roho:

"Ndugu, imetupasa kumshukuru Mungu kwa ajili yenu, kama ilivyo wajibu, kwa kuwa imani yenu inazidi sana, na upendo wa kila mtu kwenu kwa mwenzake umekuwa mwingi. Hata na sisi wenyewe twaona fahari juu yenu katika makanisa

ya Mungu kwa ajili ya saburi yenu, na imani mliyo nayo katika adha zenu zote na dhiki mnazostahimili. Ndiyo ishara hasa ya hukumu iliyo haki ya Mungu, ili mhesabiwe kuwa mwastahili kuuingia ufalme wa Mungu, ambao kwa ajili yake mnateswa. Kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwalipa mateso wale wawatesao ninyi; na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake." (2 Wathesalonike 3-7).

Wale ambao imani yao "inazidi," ambao "inawapasa" kuwapenda wenzao, wanaotambuliwa kwa "utulivu na imani" yao wanapovumulia "usaliti na dhiki" sio wakristo wenye "uongo" ambao hawako makini kuishi maisha ya imani. Au sio wakristo "kwa jina tu."

Hapana, hawa ni wakristo wa kweli, wafuasi wa kweli wa Yesu, na Paulo hakuwapotosha kwa kuamini kuwa wataishi sawa wakati wa yule mwenye dhambi. Mbona basi mtu afikirie leo kwamba wakristo wote wa kweli watachukuliwa kutoka ulimwengu huu hadi mbinguni wakati wa dhiki na wa uongozi wa yule mwenye dhambi?

Kwa kweli, wazo la kanisa kuchukuliwa ili kuepuka dhiki chini ya uongozi wa yule mwenye dhambi ilikuwa jambo geni kwa mawazo ya Paulo.

**Kanisa litakalosalia**

Katika ufunuo 12, shetani anakosa kufua dafu katika jaribio lake la kumharibu Kristo anapozaliwa (aya ya 4,5). Pia anakosa kumharibu yule "mwanamke" aliyemzaa Kristo (aya ya 13,14). Akiwa mwenye hasira, shetani akaendelea kufanya vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo" (aya ya 17).

Hawa ni kina nani (au waliosalia) wa wazao wa mwanamke? Kristo ndiye aliyekuwa mzaliwa wake wa kwanza; wengine wa wazao walikuwa ndugu na dada za Kristo – wale walioipata roho na kuwa washirika wa familia ya Mungu, ambayo ni Kanisa la Mungu aliye hai.

Wengine wa "uzao wake" ni kizazi cha mwisho wa kanisa la kweli. Washirika wa mwisho wa mwili huu ya waaminio sio wanyonge, wanaokataa sheria na

kumkumbatia Masihi ya uongo, lakini ni wale ambao wanazitii amri kumi na kuzishika kamwe mafunzo za kweli za Yesu Kristo.

Ufunuo 13 inaendeleza hadithi ya shetani akiwafuatilia watakatifu wa nyakati za mwisho. Katika sura hii, shetani anamwamuru mnyama "kutoka" katika bahari (aya ya kwanza). Mnyama huyu ana "vichwa saba na pembe kumi" na anasimamia yule asi na ufalme wake. Mnyama wa pili anapanda juu kutoka katika nchi, na ana uhusiano na yule mnyama wa kwanza (aya ya 11,12).

Mnyama wa bahari "akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa." (aya ya 6,7).

Mfalme wa mfumo huu wa ukengeufu hawezi kuwa mwingine bali ni shetani, "mwenye dhambi," mwana wa uharibifu, yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu" (2 Wathesalonike 3,4). Huyu ndiye yule "asi," ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake shetani, na uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea" (aya ya 9,10). Uwezo wake hauna mpaka katika eneo moja, lakini inafikia kila taifa la ulimwengu.

Mnyama wa nchi msujudu, "nabii wa uongo" (Ufunuo 16:13; 19:20; 20:10) aliyefanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza" (Ufunuo 13:12). Anao uwezo wa kuwaua wote wasioisujudu sanamu wa mnyama wa kwanza (aya ya 15).

Kristo anatoa ilani, "Mtu akiwa na sikio na asikie. Mtu akichukuwa mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu." (aya ya 9,10).

Shetani yule asi na mwenzake msujudu, "nabii wa uongo," hataweza kuwa na raha ilhali kunao wakristo waminifu ulimwenguni. Watawawinda kama wanyama wa pori na kuwaua wote wanaokataa kutupilia mbali amri za Mungu na uaminifu wao kwa Yesu Kristo.

Hatimaye, Kristo atamshinda yule asi pamoja na jeshi lake, na atawapa watakatifu wote uzima wa milele. Lakini kati ya sasa na wakati ujao, ni juu yetu kujitayirisha kwa nyakati ya dhiki utaabishao.

**Washahidi wawili**

Hamna mjadala kuhusu kanisa la nyakati wa mwisho linaloweza kuwa kamilifu bila ya kutaja "washahidi wawili" wa Ufunuo 11. Hatutathubutu kubadiria kuwatambua hata wakiwa katika eneo fulani hapa duniani leo, kwa kuwa wengi wamejaribu kuwatambuwa hawa viumbe wanaowazuliwa lakini wamekuwa wamekosea. Hatujui wanakotoka, taifa zao, au ukoo wala miaka yao. Tunajua tu kile ambacho maandiko yanafunua.

Badala ya kuweka sura nzima ya Ufunuo 11 hapa, tunawahimiza kuisoma kwa ujumla. Mnapoisoma, lazima mtachunguza haya:

Jukumu la hawa mashahidi wawili ni katika eneo la Yerusalemu kwa wingi (aya ya 1,2,8). Hakuna mahali popote maandishi yanasema kuwa wengine hawahubiri ukweli katika sehemu zingine. Na hata tukio la usaliti ya wale wa nyakati wa mwisho "watakaosalia" (Ufunuo 12,13) huenda lisifanyike kama watu wa Mungu wamebaki kimya katika uongozi wa yule asi.

Miujiza yanayotendeka wakati wa jukumu la manabii hawa wawili zinalinganishwa na miujiza ambazo Mungu alitenda kupitia Musa na Eliya (aya ya 6). Ujumbe wa lazima hapa ni kuwa washahidi hawa wawili wanasimamia kile majina ya Musa na Eliya zinasimamia. "Musa" anahusishwa na sehemu ya maandiko linalojulikana kama "Sheria," na "Eliya" anahusishwa na seheme ya maandiko linalojulikana kama "manabii." Manabii wawili wa Ufunuo 11, basi, wanaieneza ujumbe kamili wa sheria na manabii.

Na ujumbe kamili wa sheria na manabii ni gani?

"Akaanza kutoka Musa na manabii wote, [Yesu aliyefufuka] akawaelezea [wanafunzi wake] katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe" (Luka 24:27). Kisha akawaambia, "Hayo ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa nikali pamoja nanyi, ya kwamba ni lazima yatimizwe yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika manabii na zaburi" Baada ya

kusema hivi, “Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko” (aya ya 44,45).

Jukumu la manabii wawili wa Ufunuo 11 ni sehemu ya ushahidi wa ilani wa nyakati za mwisho. Jamii ya kimataifa watavutiwa nao (aya ya 9,10), lakini hakuna haja kuamini kuwa wao tu ndio watakao kuwa wakifanya kazi ya Mungu kupitia msimu wote wa miaka mitatu na moja unusu (aya ya 3).

**Kile unachoweza kufanya**

Baada ya kujua ya kuwa kunaye ibilisi ambaye “kama simba angurumaye, anayezunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze” (1 Petro 5:8), kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani” (1 Timotheo 4:1), tunapaswa kuwa “macho,” au katika hali ya kujitayirisha, bila ya kuchoka.

Mtume Paulo anaiweka hivi:

“Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila ya shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa injili ya amani. Zaidi ya yote mkiitwa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.” (Waefeso 6:10-18).

Mwandishi: Vance A. Stinson

Imetafsiriwa na Elijah Ogeda